# BARUA YA KRISMASI
## YA VIONGOZI WAKUU WA FAMILIA NZIMA YA WAFRANSISKO

Assisi, 25 Disemba 2020

*Watu wale waliokwenda katika giza wameona Nuru kuu; Wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti, Nuru imewaangaza. Isaya (9:1)*

**Ndugu katika Kristo,**
**Wanafamilia ya Kifransisko**

# Matumaini ni ujasiri!

Wapendwa ndugu Familia nzima ya Wafransisko,

Bwana awape amani!

Mwanga, muziki na nyimbo ni sehemu mbili muhimu kati ya nyingi katika sherehe ya Krismasi. Tommaso wa Celano, akisimulia Krismasi huko Greccio, Italia, anazungumza juu ya usiku ambao "ung'aao kama mchana na wa kufurahisha wanadamu na wanyama!" Usiku huu, "watu walikuja na kufurahi kwa furaha ambayo haijawahi kushuhudiwa hapo awali, mbele ya Fumbo lililofunuliwa. Misitu, milima na mabonde ilisikika kwa sauti za kwaya za sherehe. Ndugu wa Wafransiskani waliimba na kumsifu Mungu kwa furaha, na usiku huu ulikuwa wa shangwe na furaha". (taz. FF 469).

Sisi kama wawakilishi wakuu wa familia ya kimataifa ya Wafransisko, wakati tunasubiri kuangaziwa na Nuru itokayo juu, tungependa kuwapa, kwa lugha ya muziki, tafakari ya mambo mazuri yanayo patikana katika Ensiklika, *Fratelli Tutti* (Ndugu Wote).



# 1. KATIKA MPANGILIO WA NOTA ZA KIMUZIKI

## 1.1 Mpangilio Mpya

Tunamalizia sasa Kipindi cha Majilio, na Krismasi tayari iko kwenye upeo wa macho yetu! Kuna siku chache zilizobaki kabla ya kufikia mwisho wa mwaka, lakini sasa tunaweza kusema kwamba umekuwa mwaka maalum sana. Inaonekana kwamba katika miezi michache iliyopita tumepata uzoefu ambao ungetosha kwa muongo mzima. Virusi, mabadiliko ya kisiasa, maandamano katika nchi nyingi, mivutano, vita, michafuko na ghasia, habari za uvumi – tume fahamu kwamba ulimwengu umegeuka kuwa wa giza, na pia kwa sababu ya amri za kutotoka nje, umefungika zaidi (taz. Francesco, *Fratelli tutti* [=FT], sura ya I: *Vivuli vya ulimwengu uliofungwa*, nambari 9-55). Na haswa katika wakati huu wa kihistoria tulipokea Ensiklika *Fratelli Tutti* kutoka kwa Baba Mtakatifu Fransisko, ambapo anaelezea ujasiri wake wa kuwa na ndoto, kutamani familia ya kibinadamu iliyounganika, kumbatiyo la ulimwengu kati ya jamii yote ya binadamu, "watoto wa hii dunia inayo tuhifadhi sisi sote" (FT na. 8).

Baba Mtakatifu katika *Fratelli tutti* anaanza kwa kurejelea upendo wa kindugu aliouishi na kuukuza Mtakatifu Fransisko, upendo kwa majirani na walioko mbali; upendo pia, hata kwa viumbe vya Mwenyezi Mungu, lakini kwanza kabisa kwa "wale wapatikanao katika mwili wake mwenyewe – yaani kanisa" (FT na. 2), na kati yao, haswa maskini na wale walio wa mwisho.

Papa Fransisko pia anakumbuka maana kubwa ya ziara ya kihistoria na ya unyenyekevu ya Ndugu Fransisko kwenda kwa Sultan Malik-al-Kamil huko Misri. Fransisko wa Assisi alikutana naye kama ndugu, kama mtu ambaye ana "moyo usio na mipaka, unaoweza kuvuka mipaka ya kiasili, utaifa, rangi au dini"(FT na. 3). Papa Fransisko anakiri kwamba Mtakatifu Fransisko mwenyewe ni mjumbe mzuri wa upendo wa Mungu na "baba mwenye matunda ambayo yameinua ndoto ya jamii ya kindugu"; huu ndio uliokuwa motisha mkuu wa kuandika Ensiklika hii mpya (FT na. 4).

Halafu, hata zaidi, inapaswa kuwa motisha kwetu pia, sisi washiriki wa Familia ya Wafransisko! Tunataka kusema zaidi.

Sisi, Viongozi Wakuu wa Familia ya Wafransisko, tulikuwa Assisi, mnamo Oktoba 3, kwenye Kaburi la Mtakatifu Fransisko, wakati Baba Mtakatifu Fransisko alikuwa akiadhimisha Misa Takatifu na kutia saini waraka wake! Tuliweza kumsalimu Baba Mtakatifu kwa niaba yenu nyote. Katika nafasi hiyo ambayo Mwenyezi Mungu alitujalia, tunataka kuusoma mwaliko maalum ulioelekezwa kwa Familia nzima, na kwanza kwetu sisi, Viongozi Wakuu. Ni mwaliko wa kuchukua *Fratelli tutti* na kutazama miongozo yake kwa umakini, kama zawadi na kazi ambayo Papa anatupatia katika mwaka huu wa 2020, kama motisha uto kao kwa Mtakatifu Fransisko kupitia kwa Baba Mtakatifu Fransisko, kama mpangilio mpya wa kujifunza, kutenda na kufuatilia kazi kubwa katika historia.

## 1.2 Nota mbali mbali zinazokubaliana na matumaini

Papa Fransisko ni mhalisia, na hasiti kuita vitu kwa jina. Akichambua hali ambayo ulimwengu wa leo unajikuta (FT na. 9-55)

anazungumza juu ya "vivuli vikubwa, ambavyo havipaswi kupuuzwa" (FT n. 54). Lakini haishii hapo. Je! Nijibu gani anatoa kutokana na mateso haya ambayo wanadamu wote wanapitia? Matumaini! Na matumaini ni juu ya nini? Ni jambo ambalo linazungumza nasi "juu ya kiu, hamu, hamu ya utimilifu, maisha yaliyotimia, ya kujipima na ukuu, na kile kinachojaza moyo na kuinua roho kuelekea katika mambo makuu, kama vile ukweli, ubora na uzuri, haki na upendo. Ni ukweli kwamba "ni ujasiri, ambao unajua jinsi ya kuangalia zaidi ya faraja ya kibinafsi, usalama mdogo na fidia ambayo hupunguza upeo wa macho, kufungua malengo makuu ambayo hufanya maisha kuwa mazuri na yenye hadhi" (FT na. 55).

Lakini ni wapi matumaini hutolewa? Jibu la hiari labda ni kutokana na yafuatayo: lazima yatolewe kutoka kwa Mungu. Na hivyo ndivyo ilivyo. Chanzo cha matumaini na furaha ni Mungu na Injili yake. Papa Fransisko tayari alitaja jambo hili katika *Evangelii Gaudium*, wakati alisisitiza kwamba furaha ya kweli huzaliwa ndani ya ushirikiano kati ya Mungu na mwanadamu, kati ya Mkristo na Yesu Kristo (*Evangelii Gaudium* na. 1-8). Hii ni nota ya kwanza inayo kubaliana na matumaini - kugundua kuwa sisi ni watoto wa Mungu na marafiki zake.

Kila hatua, kila mshikamano, kila urafiki wa kijamii una msingi wake katika ugunduzi huu, kwa sababu ikiwa sisi ni watoto wa Baba yule yule, hii inamaanisha kwamba tunaishi kati ya ndugu wengine. Katika *Fratelli tutti* jambo hili linakumbukwa: matumaini sio kitu ambacho hupatikana kwa juhudi zako mwenyewe na kuishi peke yako, bila kutegemea wengine. Hapana, matumaini hujengwa pamoja, kugundua tena kama kaka na dada. Sasa ni nota ya pili inayokubaliana na matumaini – kugundua kuwa mtu hajatenganishwa, kwamba wengine wapo, kwamba sisi sote tume unganishwa na ni muhimu kujua ya kwamba "hakuna mtu anayejiokoa peke yake" (FT na. 54).

Na kwa kuwa tunaishi katika sayari hii na kwa wakati huu maalum katika historia, matumaini yetu pia yanahusu mahali tunapoishi: dunia. Baba Mtakatifu Fransisko, katika *Laudato si* '[= LS], baada ya kukiri kwamba "kuna uzorotaji wa matumaini katika nyumba zetu" anatualika tuwe na matumaini, kwa sababu "yana tualika kutambua kwamba daima kuna njia ya kutoka, kwamba tunaweza kubadilika kila wakati, kwamba tunaweza kufanya chochote kusuluhisha shida kila wakati "(LS n. 61). Nota ya tatu inayokubaliana na matumaini hivyo basi ina ladha kama ya maji safi, harufu ya hewa safi ya misitu safi na ina sauti ya msitu wa kitropiki uliojaa nyimbo za maelfu ya ndege. Nota hii inakamilisha gumzo la nota zinazokubaliana na matumaini, ambapo hakutakuwa na sauti nzuri ikiwa itakosekana, pia vile vile ikiwa moja ya nota tatu itakosekana.

## 2. KATIKA TAMASHA

### 2.1 Hoja za kwanza - uhusiano na kukutana

Katika *Laudato sì* tulihimizwa kutafakari ni ulimwengu gani tunaoutarajia siku za usoni; sayari gani tunayotarajia; katika *Fratelli tutti* inabidi kujiuliza ni uhusiano upi tunaotarajia siku zijazo. Nia ya *Fratelli tutti* ni kutualika kufahamu na kunawiri katika matumaini kwa manufaa ya dunia

ambayo “kila kitu kiko wazi”. (taz. FT sura ya III kufikiri na kuendeleza ulimwengu bila vikwazo nambari 87-127). Kwa kweli inatubidi kutafakari kuhusu sisi ni kina nani, utume, na kwa hivyo pia juu ya malezi yetu. Tunapofikiri hizi nia katika familia yetu ya wafransiskani tunaweza tukajiuliza: sisi ndugu wafransiskani tunatarajia nini katika siku zijazo maishani mwetu, maadili gani, mtindo na mawazo yetu tunayokusudia kuwakabidhi watakao kuja baada ya sisi? Tafakari ya hayo, na juu ya yote, ni aina gani ya uhusiano ambao tunatoka ndani ya maisha yetu wa Wafransisko? Na, mwishowe, Je? Tunataka ulimwengu wetu wa Kifransisko ufikiwe na uwe wazi kwa wote?

Katika *Laudato sì* tulielezwa ya kwamba dunia ni mtandao wa uhusiano (inabidi kukumbuka “uhusiano” ni nguzo kuu katika maisha ya wafransiskani), ambapo kila kitu kimeunganishwa (taz. LS na. 117); katika *Fratelli tutti* tunaelezwa ya kuwa huu mtandao wa uhusiano unaendelea kudhoofika; kuna tishio la kutengwa; lakini tunapata matumaini katika kukuza utamaduni wakukutana. (taz. FT na. 30).

Tunaweza kukuza vipi utamaduni wa kukutana? *Baba Mtakatifu* Fransisko anatukumbusha ya kwamba: katika kubadilisha mwenendo pana haja ya motisha na kunawiri katika malezi (LS na. 15) yanayoambatana na “hazina ya maisha ya kiroho katika Ukristu.” (LS na. 15) na tunaweza sema hata hazina ya Kifransisko. Tunatambua umuhimu wa kuwa na nia na mwelekezo katika *ratio formationis*, na tena katika *ratio studiorum*, hoja mwafaka zinazoeleweka katika malezi ya ubinadamu, kijamii na mazingira tukifuata mapenzi ya Papa. Inatubidi kufikiri kwa kweli jinsi tunaweza kujumlisha katika malezi yetu ya utawa utamaduni wa kukutana. Ukaribu katika uhusiano huleta wokovu sio tu kwa mtu binafsi lakini hata kwa familia yake na ulimwengu kwa jumla.

## 2.2 Hoja za awali - umakini na mazungumzo

*Baba Mtakatifu* Fransisko anapoeleza mfano wa Msamaria mwema anatukumbusha ya kwamba “sote tunazingatia mahitaji yetu” (FT na. 65). Kwa hiyo kuna uwezekano tukajumulishwa katika orodha ya yule kuhani na mlawi wasiojali “Mtu aliyejeruhiwa, amelala chini kando ya barabara, ambaye alikuwa ameshambuliwa” (FT na. 63).

Kigezo cha kufahamu jinsi tunavyowajali wengine ni “tunapowaona wanaoteseka tunapata kuudhika, kusumbuka kwa sababu hatutaki kupoteza muda kuwajali wengine.” (FT na. 65). Mojawapo ya matakwa bora ya kufanya, na sio tu kwa msimu huu wa Krismasi, kwa hivyo ni kuwa na ujasiri zaidi kuiga “mfano wa Msamaria mwema” (FT na. 66) na kuajibika “katika wito wetu kama raia wa nchi yetu na dunia nzima, pia kukuza ushikamano wa kijamii” (FT na. 66). Kuna uwezekano “tusipo makinika, kuchagua upande wa wahalifu au wale wanaopita bila huruma kwa maumivu ya mtu aliyejeruhiwa njiani.” (FT na. 67). Kwa hamu hii, swali lingine linaibuka: tunawezaje kuwa na mawazo ya ubunifu bila kuteleza “katika jamii inayotengana” lakini “kumiliki udhaifu wa wengine.” (FT na. 67)? Je! Tunawezaje kuwa waangalifu zaidi kwa wengine? Je! Tunawezaje kuwa na ujasiri zaidi angalau kuwakaribia? (tazama nambari za FT na. 233-235).

Baba Mtakatifu Fransisko, akiongea juu ya chanzo cha msukumo kwa waraka *Laudato si'* anaonyesha, pamoja na Mtakatifu Fransisko, "Patriaki mpendwa wa Kiekumene Bartholomew" (LS na. 7). Akizungumzia chanzo cha msukumo wa *Fratelli tutti*, anakiri mchango wa Imam Mkuu Ahmad Al-Tayyeb (taz. FT na. 29). Pamoja na hayo, anatoa mfano halisi unaoangazia umuhimu wa mazungumzo ambayo Wakristo, kuanzia nafsi yao isiyobadilika (taz. FT na. 3), wameitwa kutafuta pamoja "na watu wote wenye mapenzi mema" (FT na. 6). Kama ndugu wa Kifransisko, tayari tumehusika katika mazungumzo haya katika sehemu na njia tofauti; lakini labda tunaweza kujiuliza jinsi ya kuongeza nafasi za mazungumzo na kukutana na watu wote, na haswa wale ambao hawashiriki imani yetu, lakini ambao mara nyingi wanaishi na kufanya kazi pamoja na sisi.

Mtakatifu Fransisko aliacha kielelezo cha vitendo - mtu anaweza kuanza na salamu: Bwana akupe amani! (taz. FF na. 121). Kila unapotumia salamu hii inakubidi "umwone" mwenzako. Na kisha, salamu hufungua mazungumzo. Tukumbuke, hata hivyo, kwamba salamu ya Mtakatifu Fransisko imeelekezwa kwa wote, kwa kiwango sawa na kwa fadhili sawa (taz. pia FT, na. 222-224). Bila ubaguzi, kwa sababu katika kila mmoja alimtambua kama ndugu, na alijua kuwa moyoni mwa Mungu hakuna anayedharauliwa.

## 2.3. Katika shule ya Muziki

Tumepokea kutoka kwa Baba Mtakatifu Fransisko mpangilio mpya wa mziki ili tujifunza. Wimbo unaonekana kuwa mgumu, lakini tunajua kwamba nyimbo zote zinaonekana kuwa ngumu mwanzoni. Nota baada ya nota, mstari baada ya mstari, polepole tunapata uwezo wa utendaji mzuri. Wimbo mpya unaelezea ndoto ya ulimwengu ulio wazi, wa ulimwengu ambao mkutano unapewa kipao mbele, ambapo mitindo mipya ya maisha, njia mpya za kuangalia na kufikiria zinawezekana. Sisi pia tunawajibika kwa utendaji wa kipande hiki; kwa hivyo ni muhimu kutengeneza michakato ya ndani (*ad intra* katika shirika, kwa mfano, katika malezi) *ed extra* (katika huduma yetu kwa ulimwengu), michakato ambayo inaweza kusaidia kuingiza fikra ya muziki uliofichwa kwenye mpangilio mpya wa *Fratelli tutti.*

Ni wapi tunaweza kujifunza maelezo ya kipande hiki kipya cha muziki? Wakati wa Krismasi unatusaidia na unatualika kuhudhuria shule bora ya muziki. Mtakatifu Fransisko alitilia mkazo ya kwamba Krismasi ni wakati mzuri wa kufanya mazoezi, kwa kweli: "Siku hiyo Bwana alituma huruma yake na katika usiku ule pia wimbo wake" (taz. FF 303). Mkutano unafanyika huko Bethlehemu. Ni Mungu mwenyewe ambaye anachangia utamaduni wa kukutana na anajifanya jirani: mmoja wetu. Mwanzo wa mazungumzo, mwanzoni bila maneno, kutazama tu kwa macho - (lazima ilivutia - na Mariamu wa Nazareti hakika alishiriki- kutazama, kwa mara ya kwanza tangu kuumbwa kwa ulimwengu, machoni pa Mungu) - Mungu, kwenye sikukuu ya Krismasi Yeye hutupa uso wake, kwa sababu "hakuna mtu anayeweza kupata thamani ya maisha bila nyuso halisi za kupenda" (FT na. 87). Yeye ndiye wa kwanza kufundisha jinsi ya kuishi maisha ya kinabii na ya kutafakari, katika furaha bila wasiwasi wa mambo ya dunia.

Hapa, chanzo cha nafsi yetu; hapa ndipo pa kujifunza maana ya uwiano na wale ambao wako mbali na ni tofauti na sisi. Mwanzo wa malezi yetu ni hapa: kutokana na kutafakari uso wa Yesu Kristo, mtoto aliyevalishwa na Maria na kukumbatiwa na Yusufu. kwa uso huu tunaweza kutafakari Mungu ni upendo (1 Yn 4:16); Upendo ambao hujitoa kikamilifu na kwa uwazi, ukijua hitaji letu la wokovu, umekuja kuwa nasi. "Mtoto mtakatifu mpendwa zaidi, ambaye tumepewa sisi na alizaliwa kwa ajili yetu njiani na akawekwa kwenye hori" (taz. FF 303), ni Neno ambalo kupitia kwake Baba huongeza mazungumzo kwa wanadamu wote; Neno ambaye alikuja kuwa mwili ili kufanya mazungumzo na alikuja kukaa kati yetu (Yoh 1:14).

Hapa ndipo chanzo cha matumaini kilipo. Ni mahali ambapo Mungu yuko na, wakati huo huo, ni mahali ambapo ndugu wapo: ni Yeye ambaye alikuja, ili kuishi pamoja nasi.

Sisi pia, Viongozi Wakuu katika Familia ya Kifransiskani, tunataka kuchangia katika makubaliano ya matumaini, uhusiano na kukutana, umakini na mazungumzo, katika shule ya Mungu: "Mtoto wa Bethlehemu" (taz. FF 470). Tunafanya hivyo na barua hii ya pamoja ya kuwatakia sherehe njema za Krismasi: tunawatakia ninyi nyote kwa pamoja, Krismasi hii maalum, muwe na ujasiri wa kutaka kusikia kila wakati, kila mahali, katika kila hali, na kila mmoja, ndugu na dada, wimbo wa malaika wanaotangaza: "Utukufu kwa Mungu Juu, na amani duniani kwa watu wenye mapenzi mema!" (taz. Lk 2, 14).

Deborah Lockwood OSF
*Rais wa IFC-TOR*

Tibor Kauser OFS
*Mkuu wa Shirika*

Michael Anthony Perry OFM
*Mkuu wa Shirika*

Roberto Genuin OFMCap
*Mkuu wa Shirika*

Carlos Alberto Trovarelli OFMConv
*Mkuu wa Shirika*
*Rais wa Mkutano wa Familia ya Wafransisko*

Amando Trujillo Cano TOR
*Mkuu wa Shirika*

Prot. N. 015/2020 Picha: *Uanzishwaji wa Hori la Yesu*, Greccio, Italia.